**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Nafasi Ya Fasihi Andishi Ya Watoto Kama Chombo Cha Malezi Kwa Watoto Wa Kisasa

*Dkt. Naomi Nzilani Musembi, PhD[1*] na Dkt. Peter Karanja, PhD[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia, S. L. P. 210 – 40601, Bondo, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Gretsa, S. L. P. 3-01000 Thika, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: omisembi@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*13 Mei 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Mtoto, Fasihi ya Watoto, Chombo cha Malezi, Malezi.*

**IKISIRI**

Fasihi andishi ya watoto ina nafasi kubwa ya kuwasaidia watoto kuelewa mazingira yao pamoja na kujenga mwonoulimwengu wao kulingana na wanachosoma. Hii ni kutokana na sababu kwamba watoto hubwia wasomacho kuwa kiwakilishi cha uhalisia katika jamii. Fasihi ya watoto huchokoza fikra zao na kuwachochea kufikiria, kuimarisha msamiati wao, na pia huwasaidia kujifahamu kando na kuwafahamu watu wengine. Fasihi hii hivyo basi inajitokeza kama kioo ambacho watoto wanajiona kwacho na pia dirisha la kuwawezesha kuutalii ulimwengu unaowazunguka. Fasihi andishi ya watoto vilevile ina uwezo wa kuonyesha kuwa, watu tofauti wanaweza kufanya kazi pamoja bila ubaguzi wa aina yoyote. Waandishi wa fasihi ya watoto hivyo basi hubuni ulimwengu ambao watoto wanaweza kuutambua kwa urahisi na kujinasibisha nao. Kwa msomaji mtoto, hali hii hurahisisha uvushaji wa maarifa na kuifanya fasihi andishi yao kuwa nyenzo muhimu ya kuimarisha mtagusano wa kijamii pamoja na uvushaji wa maarifa ya kiakademia. Lengo la makala hii ni kubainisha kuwa, kupitia fasihi andishi ya watoto ya Kiswahili, msomaji mtoto anaweza kufafanukiwa na hali halisi ya maisha yake na wakati huo huo kupata suluhu ya kutatua matatizo yanayomkumba na ya jamii yake. Kazi hii itafanya hivyo kwa kuhakiki vitabu vya fasihi andishi ya watoto vifuatavyo: Momanyi, C (2006) Tumaini, Momanyi, C. (2005), Siku ya Wajinga, Musembi, N. (2009) Nipe Sababu, Musembi, N. (2019) Dhiki Yangu Ngugi, P. (2003) Usicheze na Moto Mdari, A. (2001) Alitoroka kwao. Ndoto ya Mwanafunzi, Manji, M (2013), na Safari ya Sungura Omusikoyo T, ( 2021). Makala hii inatoa mwito kwa waandishi wa fasihi ya watoto watunge vitabu vitakavyo wasaidia watoto kukabiliana na hali zote za maisha yao wanapoendelea kukua katika dunia hii inayobadilika kila uchao.

**APA CITATION**

Musembi, N. N. & Karanja, P. (2024). Nafasi Ya Fasihi Andishi Ya Watoto Kama Chombo Cha Malezi Kwa Watoto Wa Kisasa. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 224-232. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924.

**CHICAGO CITATION**

Musembi, Naomi Nzilani and Peter Karanja. 2024. "Nafasi Ya Fasihi Andishi Ya Watoto Kama Chombo Cha Malezi Kwa Watoto Wa Kisasa". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 224-232. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924.

**HARVARD CITATION**

Musembi, N. N. & Karanja, P. (2024) "Nafasi Ya Fasihi Andishi Ya Watoto Kama Chombo Cha Malezi Kwa Watoto Wa Kisasa", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 224-232. doi: 10.37284/jammk.7.1.1924

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924

**IEEE CITATION**

N. N. Musembi & P. Karanja “Nafasi Ya Fasihi Andishi Ya Watoto Kama Chombo Cha Malezi Kwa Watoto Wa Kisasa”, *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 224-232, May. 2024.

**MLA CITATION**

Musembi, Naomi Nzilani & Peter Karanja. “Nafasi Ya Fasihi Andishi Ya Watoto Kama Chombo Cha Malezi Kwa Watoto Wa Kisasa”. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, May. 2024, pp. 224-232, doi:10.37284/jammk.7.1.1924.

## UTANGULIZI

Fasihi yoyote ile huzalika kutokana na hali ya jamii na kwa wakati wake (Ngugi, 2016). Jinsi jamii inavyobadilika ndivyo fasihi inavyofaa kubadilika ili iweze kuyamulika masuala mapya yanayoibuka katika jamii. Musembi (2018) anashikilia kuwa, fasihi nzuri ni ile yenye kuadilisha, kuelimisha, kuonya, kutoa matumaini, kuliwaza, kushauri na kuimarisha ujenzi wa jamii imara yenye uadilifu. Waandishi wa fasihi ya watoto wamekuwa mbioni katika kuangazia masuala mbalimbali katika mazingira ya mtoto ili kujaribu kutahadhalisha, kuelimisha, kuonya, kuasa na kuadilisha watoto. Fasihi ya watoto ina utendakazi mkubwa katika kuwapelekea watoto kujenga mwonoulimwengu wao (Mbuthia, 2018). Mwanzi naye (2006) anatilia uzito majukumu makubwa yanayotekelezwa na fasihi ya watoto kwa kusema kuwa, kwa miaka na dhahari, binadamu ametumia fasihi kukipokeza kizazi chipukizi maadili ya kuwasaidia kuishi na kufanikiwa. Kulingana na Mwanzi, fasihi andishi ya watoto ni mbegu ya kuendeleza kizazi cha baadaye. Kutokana na maoni ya wataalamu waliotajwa, inabainika wazi kwamba, fasihi ya watoto ni nyenzo muhimu ya kuwasaidia watoto kuelewa mazingira yao, umuhimu wa elimu, mila na tamaduni zilizopitwa na wakati na zinazowabagua, hatari ya unyanyapaa, hatari ya utundu miongoni mwa masuala mengine mengi.

Jamii zetu zimekumbwa na matatizo mengi hususan magonjwa yasiyo na tiba kama Korona na Ukimwi, uraibu wa dawa za kulevya, magonjwa ya kiakili, ukame, vita vya wenyewe kwa wenyewe, ukabila, mimba za mapema miongoni mwa wasichana wa shule za msingi na za upili, unyanyasaji wa wanawake na wanaume, unyanyasaji wa watoto, unyanyapaa miongoni mwa matatizo mengine. Ili kupambana na hali hizi ngumu, ni muhimu kuwa na nyenzo mwafaka zinazoweza kutumiwa kukabiliana na hali hizi. Fasihi andishi ya Kiswahili ya watoto ni miongoni mwa nyenzo mwafaka kwani kupitia kwayo, ujumbe huweza kuwasilishwa kuhusiana na namna ya kukabiliana na matatizo haya ya kijamii. Hivyo basi, makala hii inanuia kutanua fasihi andishi ya Kiswahili ya watoto kama silaha muhimu ya kuchangia katika malezi ya watoto.

### Sababu za Kuchagua Mada

Makala hii ilichochewa na watafiti kama Ngugi na Nabea (2011) ambao walitoa wazo kwamba fasihi ya watoto ya Kiswahili nchini Kenya imeimarika na kupanuka hadi kukaibuka hadithi za watoto zinazoangazia masuala ibuka yanayoikabili jamii. Masuala ibuka hayo yanahusu magonjwa yasiyo na tiba kama Ukimwi, utumizi wa dawa za kulevya, ajira ya watoto, ukiukwaji wa haki za watoto, usawa wa kijinsia, afya, mikasa miongoni mwa masuala ibuka mengine. Fasihi ya watoto hutoa mchango mkubwa katika kukuza taswira wanayokuwa nayo watoto kujihusu wao wenyewe na kuhusu mwonoulimwengu wao. Aidha, hutoa mchango mkubwa kuhusiana na namna ambavyo watoto wenyewe wanahusiana na wanajamii wengine katika mazingira yao, hukuza utamanduni wa Mwafrika, na turathi za utamaduni huo. Vilevile, huwapa watoto maarifa na ukweli kuhusu hatua ya maendeleo iliyopigwa katika jamii zao. Kwa msomaji mtoto, hali hii hurahisisha uvushaji wa maarifa na kuifanya fasihi andishi yao kuwa nyenzo muhimu ya kuimarisha mtagusano wa kijamii pamoja na uvushaji wa maarifa ya kiakademia. Hii ni kutokana na sababu kwamba watoto hubwia wasomacho kuwa kiwakilishi cha uhalisia katika jamii. Wataalam wa maswala ya saikolojia ya watoto wameonyesha kwamba ukongomelevu wa tabia za mtu zina chanzo chake utotoni. Hivyo basi, makala hii inapania kutanua fasihi andishi ya watoto kama chombo kiaminifu cha kuwajenga

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924

watoto kitabia, sawia na njia nyingine ambazo wazazi na walezi hutumia katika kuwakuza watoto kitabia.

### Mchango wa Makala Hii

Makala hii ni mchango muhimu katika taaluma ya fasihi ya watoto. Hii ni kutokana na sababu kwamba, inaangazia dhima ya hadithi za watoto kama wenzo wa maarifa ambayo yatawawezesha kuelewa ulimwewngu wao wanapokua. Vilevile, kazi hii itakuwa na mchango katika ufundishaji wa fasihi ya watoto hasa kuhusiana na mchango wa fasihi hii katika malezi ya watoto katika dunia ya sasa inayobadilika kila uchao.

## NAFASI YA FASIHI ANDISHI YA KISWAHILI YA WATOTO KATIKA MALEZI

Ndungo (1985) na Musembi (2008) wanasema fasihi nzuri ni kielelezo cha hali halisi ya maisha katika jamii. Msanii kulingana na wataalamu hawa hutunga kutokana na tajriba anayoipata katika jamii anamoishi. Kazi nyingi za fasihi huweza kueleweka kupitia maudhui yake yanayohusu jamii wakati fulani. Akishikilia kauli hiyo, Wamitila (2008) anasema fasihi haitoki katika ombwe tupu. Inapata mwelekeo, umbo na umuhimu wake kutoka kwa maswala ibuka katika jamii mahususi. Kwa mujibu wa Wamitila, maswala yanayoipa fasihi mwelekeo ni pamoja na elimu, dini, uchumi, siasa pamoja na mabadiliko yatokeayo katika nyanja zozote za maisha ya jamii. Kutokana na mantiki hii, sehemu ifuatayo itashughulikia majukumu ya fasihi andishi ya watoto kama nyenzo muhimu katika malezi ya mtoto.

### Fasihi andishi ya Watoto Huelimisha

Fasihi andishi ya watoto ina majukumu mengi ya kuelimisha mtoto kuhusu mambo mbalimbali hususan umuhimu wa masomo, elimu kuhusu mila na tamaduni potovu ambazo humbagua mtoto wa kike, umuhimu wa mazingira safi ambayo hayajachafuliwa, usafi wa mwili, hatari ya kuwasha moto, hatari ya kuchokoza nyuki miongoni mwa masuala mengi mengine ambayo mtoto atayabwia na kuyakongomelea kwa akili yake hadi utu uzima wake. Ngugi (2016) anaeleza kuwa, kila wakati msomaji mtoto anaposoma kazi ya fasihi, ana nafasi ya kugundua jambo jipya. Maana anazopata msomaji mtoto zinaathiriwa na mazingira pamoja na tajriba yake

Fasihi ya watoto husheheni maarifa ya kiakademia na maarifa kuhusu ulimwengu kwa jumla. Hivyo basi, katika kufanikisha uvushaji wa maarifa, msomaji mtoto huenda akabwia ujuzi huu kupitia kujinasibisha na wahusika fulani katika kazi wanazozisoma. Momanyi (2006) katika kitabu cha watoto Tumaini ameangazia suala la umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike kupitia msichana aitwaye Tumaini. Babake Tumaini mzee Mazumbuko anapania kumwachisha shule Tumaini ili amuoze kwa mzee ambaye ana mali mengi (uk. 44). Tumaini anapogundua mpango wa babake wa kumkeketa na kumuoza anatorokea kwa mamake mdogo Bi. Halima ambaye ni mwanaharakati wa kutetea watoto wa kike dhidi ya mila na utamaduni wa ukeketaji na ndoa za mapema. Kutokana na hatua hii anayochukua Tumaini, mwishoni tunamuona akisomea masomo ya sayansi ili akifika chuo kikuu asomee mafunzo ya udaktari (uk. 96). Mwandishi wa kitabu hiki cha watoto anapania kupitisha maarifa kwa watoto kuhusiana na umuhimu wa masomo. Masomo hubadilisha maisha ya mtu kwa njia kadhaa. Mosi, mtu ambaye ana elimu huweza kupata ajira na kupitia ajira hiyo, anaweza kuishi maisha mazuri. Pili, kupitia elimu, mtu huweza kujikinga kutokana na mila potofu kama mimba za mapema, ndoa za mapema, magonjwa miongoni mwa mengine. Tukiangazia maisha ya Tumaini, yeye ni tofauti na dada zake waliokosa elimu kwa sababu ya tamaa ya baba yao Mzee Masumbuko. Mzee Masumbuko alipokea mahari ya Mashaka na kumuoza kwa lazima kwa Mzee Lusimbo kama mke wa tatu. Ndoa hiyo ilimsababishia Mashaka madhara makubwa ya kimwili na ya kiakili pia (uk.96). Mzee Lusimbo alikuwa na u Kutokana na mwanya mpana wa kiumri kati ya Mashaka na mzee Lusimbo, ambaye alikuwa na umri sawia na babake Mashaka,, wakawa hawasikilizani kabisa. Kutokana na madhila aliyopata Mashaka katika ndoa yake, tunaambiwa;

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924

> *"… ufyevye ulimvaa Mashaka, vibega vikainuka juu kama vya ndege… alivyowazia hali ya dadake, Tumaini alisema kimoyomoyo, laity anagalijua umuhimu wa masomao, haya hayangemfika* (uk. 96).

Dadake mwingine wa Tumaini aitwaye Rehema naye alihiari kuolewa na Shauri. Kutokana na umri wake mdogo, akapata matatizo makubwa wakati wa kujifungua mtoto wake wa kwanza. Matatizo haya yanayowakumba dada zake Tumaini hayakumpata yeye Tumaini kutokana na uamuzi wake wa kutoroka kisu cha ngariba ili aweze kusoma mpaka chuo kikuu kama mpwa wake Riziki. Hivyo, kitabu hiki ni muhimu katika kuwaelimisha wasichana umuhimu wa kusoma. Aidha kinamuelimisha mtoto msomaji kuhusiana na mila na tamaduni potofu za kijamii pamoja na madhara yake kwa mtoto wa kike. Madhara haya ni pamoja na ukeketaji na ndoa za mapema.

Kitabu kingine ambacho kinamuelimisha mtoto ni *Nipe Sababu* (2009) cha Musembi Mwandishi anawaelimisha watoto wa kiume dhidi ya kujiingiza katika hatari ya kuwachokoza nyuki. Vijana watatu Katu, Safari na Chalii wanajipata matatani walipochokoza nyuki mzingani wakiwa katika harakati za usasi. Wanadungwa vibaya na nyuki na kuumizwa sana. Tunaambiwa vijana hao walikuwa wamefura uso kiasi cha kutotambulikana. Babake Katu baada ya kuwapa huduma ya kwanza na kuokoa uhai wao anawaelimisha kuhusu umuhimu wa nyuki. Anawakumbusha watoto hao kwamba nyuki ni kitega uchumi kwao kutokana na sababu kwamba mauzo ya asali wanayorina huwapa natija kubwa ya pesa. Anawaelimisha pia kuhusiana na umuhimu wa kuhifadhi mazingira safi na upanzi wa miti kwani nyuki hupata chakula chao kutoka kwa maua. Hii ni elimu nzuri kwa watoto. Wanapokua, elimu hii inawasaidia katika maisha yao ya baadaye kuhusiana na umuhimu wa upanzi miti na kilimo cha nyuki.

Vilevile, Ngugi (2003) kupitia kitabu cha watoto *Usicheze na moto* anawaelimisha watoto hatari ya moto kwani moto huweza kuchoma makazi ya watu kwa muda mfupi sana. Aliya na wenzake walipowasha moto ili wapike viazi moto huo uliweza kutanda na kuchoma ghala la nafaka lililokuwa na magunia mengi ya mahindi na maharagwe. Watoto kupitia kitabu hiki wanapata welewa wa hatari ya moto na kujiambaa nayo. Elimu hii inakongomelea kwa akili zao hata katika utu uzima wao.

**Fasihi andishi ya Watoto Hutahadharisha**

Hunt (2001) anasema kuwa fasihi ya watoto ni muhimu kwa vile ina uwezo wa kuwashawishi watoto kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja kilugha, kitamaduni, na kimaadili wanapokua. Hunt anaeleza kuwa, watu wazima waliosoma vitabu vya fasihi ya watoto walipokuwa wadogo, wamefaidika na maarifa waliyopata kutokana na vitabu walivyovisoma kutokana na sababu kwamba, vilikuwa na ushawishi fulani katika ukuaji wao. Hunt anatoa hoja kuwa, vitabu vya watoto hutumika kuwafahamisha na kuelekeza mitazamo ya watoto kuhusiana na masuala mbalimbali katika jamii yao wanapokua. Maoni ya Hunt yanaoana na ya Matundura (2007) anaposema kuwa, awamu ya utoto ni awamu muhimu ya kukua ambapo baadhi ya mambo ambayo mtoto hujifunza hukongomelea akilini mwake na hujitokeza mtu anapokuwa mzima. Hivyo basi, nafasi ya fasihi andishi ya Kiswahili ya mtoto ina jukumu muhimu ya kutahadharisha mtoto kutokana na masuala mbalimbali anapokua.

Vitabu vingi vya fasihi ya watoto vimeshughulikia jukumu hili. Kupitia kitabu cha *Ndoto ya Mwanafunzi*, cha Manji (2013), masaibu yanayowakumba vijana wawili Juma na Hamisi walipoamua kuwa *mastowaways* na kuabiri meli iliyokuwa ikielekea Bara Uropa ni tahadhari kwa mtoto msomaji. Juma na Hamisi hawakufika Bara Uropa kama walivyotarajia kwani meli waliyokuwa wamejificha karibu na injini ilitia nanga katika ufukwe wa nchi ya Mauritius. Wakifikiria wamefika Bara Uropa, waliamua kutoka mafichoni mwao na kuogelea kuelekea ufukweni lakini wakaonekana na walinda usalama ufukweni. Walikuwa wamedhoofika mno kiafya hivyo baada ya kupelekwa hospitali kupata matibabu walipelekwa kortini na kushtakiwa na kufungwa kifungo cha miezi kadha. Masaibu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924

yaliyowapata vijana hawa ni tahadhari kwa wengine. Mtoto msomaji atapata kujua hatari ya kuwa *stowaway* kwani watoto wengi hufikiria kwamba wanaweza kuabiri vyombo vya majini kwa kujificha ili wafike nchi nyingine.

Aidha, kitabu cha watoto *Dhiki Yangu* cha Musembi (2019) kina dhima ya kutahadharisha mtoto msomaji kutokana na tabia ya unyanyapaa kwa watoto wenzake shuleni na pia wanajamii wengine. Kiambi ni muhusika mkuu katika kitabu cha *Dhiki yangu*. Kwao nyumbani babake ni mkulima na anafuga nguruwe. Nyumbani kwa Kiambi ni karibu na barabara na steji ya magari za umma. Kibanda cha nguruwe hao hunuka sana na mnuko huo huwasumbua wapiti njia sana. Watoto katika shule ya msingi ya Kajiweni anakosomea Kiambi wanachukia janibu za karibu na kwa Kiambi. Wao hupita kama wameziba mapua. Ni kutokana na nguruwe hao ambapo unyanyapaa kwa Kiambi ulianza. Watoto watundu wakaanza kumuita Kiambi pig na kumchora ubaoni akiwa na pua kama la nguruwe. Unyanyapaa huu ukamuathiri Kiambi sana masomoni mpaka naibu mwalimu mkuu alipoukomesha kwa kuwaadhibu vikali vijana watundu waliohusika na unyanyapaa huo kwa Kiambi. Adhabu yao ilikuwa kuosha nguruwe wa shule yao kwa mda wa wiki nzima kila asubuhi na njioni. Wakaanza pia kununuka kama nguruwe na kuchekwa sana na wenzao darasani. Kupitia adhabu hii, mtoto msomaji anatahadharishwa kuhusiana na unyanyapaa wa aina yoyote ile. Tahadhari hii ina uwezo wa kukongomelea katika akili ya mtoto msomaji mpaka utu uzima wake.

Kitabu cha watoto *Usicheze na Moto* cha Ngugi (2003) pia ni muhimu kwa mtoto msomaji. Watoto mara nyingi hucheza michezo yao inayohusu majukumu ya kiuana kama wanavyobwia kutoka mazingira yao ya nyumbani. Moja ya majukumu haya ni kupika hasa kwa watoto wa kike. Katika harakati za kupika wanawasha moto ili wautumie kupika kama wanavyoona nyumbani. Katika kitabu hiki, Aliya, Aida na Dodo wanaamua kucheza mchezo wa kupika na wanaamua kupika viazi. Wakakusanya kuni na kuzipanga katikati ya mafiga. Kisha wakawasha moto. Wakisubiri viazi view yayari, walianza michezo mingine. Karibu nay ale mafiga kulikuwa na ghala la nyasi kavu, miti na makuti. Ghala lilikuwa limejaa magunia ya mahindi na maharagwe. Upepo mkali ulivuma na kusababisha cheche za za moto kuruka mpaka kwenye ghala ambalo lilishika moto. Hasara kubwa ilitokea kwani magunia yote ya mahindi na maharagwe yaliungua yakawa makaa. Kisa hiki kinatahadharisha mtoto kuhusu hatari ya kuwasha moto. Aliya aliyewasha ule moto alijuta. Tunaambiwa;

> *"Tangu mkasa huo wa moto utokee, Aliya alikuwa mwangalifu sana. Aliamua kuwa hatawasha wala kucheza na moto tena. Aliyakumbuka maneno aliyoambiwa na wazazi wake. Alijifunza kuwa moto si dhihaka. Si kitu cha kucheza nacho. Moto huteketeza, huchoma na huunguza vitu na watu. Moto huua, moto haujui rafiki au adui. Moto ni hatari"* (Uk. 24).

Hili ni funzo muhimu kwa watoto ambalo lina nguvu la kukaa katika akili ya mtoto hadi utu uzima wake. Jukumu la fasihi andishi ya watoto la kutahadharisha watoto dhidi ya mikasa kama kuwasha moto ni muhimu sana kwani huweza hata kuhatarisha maisha ya mtoto mwenyewe.

Vilevile, kitabu cha *Tumaini* cha Momanyi (2006) kina jukumu kubwa la kutahadharisha watoto hasa wa kike dhidi ya ndoa za mapema. Kinafanya hivyo kwa kutumia wahusika watoto kama Mashaka na Rehema. Mashaka na Rehema ni dada zake Tumaini amabaye ndiye muhusika mkuu katika kitabu hiki. Mashaka japo alilazimishwa na babake Mzee Masumbuko kuolewa na kifefe cha mzee kama mke wa tatu anapata madhara si haba ya kimwili nay a kiakili. Mzee huyo twaambiwa alikuwa na umri mkubwa sawa na babake Mashaka. Kwa hivyo wakawa hawasikilizani kabisa (uk. 56). Mashaka alisononeka mno. Aidha, alipata taabu ya uzazi kutokana na umri wake mdogo. Alizaa watoto watatu wote kwa njia ya upasuaji (uk. 56). Isitoshe, wake wenza twaambiwa walikuwa hawaachi kumbughudhi. Sio Mashaka tu aliyepata matatizo kutokana na ndoa yake. Pia Rehema

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924

dadake pia aliyeolewa akiwa mdogo alipata matatizo chungu nzima wakati wa kujifungua kutokana na umri wake mdogo. Kupitia wasichana hawa, mtoto msomaji hasa msichana anapata tahadhari ya kujiingiza katika ndoa za mapema. Ile taswira ya taabu iliyowapata Mashaka na Rehema inakuwa gundi inayonata katika akili ya mtoto msomaji. Pia, kitabu cha *uhalifu haufai* cha Omolo (1971) ni tahadhari kwa mtoto kuhusiana na uhalifu wa aina yoyote ile kwani kupitia kwacho, hatima ya wahalifu ni jela.

**Fasihi andishi ya Watoto Huonya**

Fasihi andishi ya watoto ina dhima muhimu ya kuwatolea watoto onyo ili wasijiingize katika hatari yoyote ile. Hadithi kadha zimetungwa na waandishi wa fasihi ya watoto zikiwa na lengo la kuwaonya watoto na kuwatahadharisha dhidi ya vitendo hatari kwa usalama wao hususan; kitabu cha watoto *Nipe Sababu* cha Musembi (2009). Hadithi hii inawaonya watoto na kuwatahadharisha dhidi ya kuchokoza nyuki mizingani. Hii ni kupitia madhara yaliyowapata vijana watatu Katu, Safari na Chalii walipochokoza nyuki mizingani wakati wakiwinda. Hata baada ya kuumizwa vibaya na nyuki, babake Katu alipania kumpa adhabu nyingine ya kichapo ili kumuonyesha mwanawe uzito wa tabia ya kuchokoza nyuki ambao kupitia kwao, Katu na familia yake walikuwa wakipata natija kubwa wakiuza asali.

Vilevile, hadithi ya *Usicheze na Moto* ya Ngugi (2003) inawaonya na kuwatahadharisha watoto dhidi ya kuwasha moto wakicheza kwani moto una madhara makubwa. Babake Aliya alitaka kuwapa kichapo watoto waliohusika na kuwasha moto uliochoma ghala na kusababisha uharibifu mkubwa. Baada ya babake Aliya kumweleza hatari ya kucheza na moto, tunaambiwa tangu mkasa huo wa moto, Aliya alikuwa mwangalifu sana sawia na walivyoapa akina Katu kutojihusisha na kuchokoza nyuki tena.

Aidha, katika hadithi ya *Dhiki Yangu* na Musembi (2019), Kiambi mtoto wa darasa la tano anakejeliwa na kudhihakiwa na baadhi ya wenzake shuleni kama Mwamba. Wanampachika jina *Pig* kutokana na sababu kwamba yeye Kiambi amewanda na pia kwao wanafuga nguruwe. Kila mara Mwamba anamchora ubaoni akifanana na nguruwe. Wakati kisa cha kwanza cha ugonjwa wa homa ya nguruwe (H1N1) kiliporipotiwa nchini, masaibu ya Kiambi yakaongezeka kutokana na baadhi ya wenzake kujiambaa naye eti atawaambukiza homa hiyo kutoka kwa nguruwe wao. Bw. Katu mwalimu wa zamu ndiye aliyekomesha unyanyapaa huu alipomwaalika maafisa wa afya kuzungumzia chanzo cha homa hii. Pia, Mwamba akaadhibiwa vikali kupitia kuosha ngurue wa shule mara mbili kwa siku. Adhabu hii ikawa onyo kwake na kwa wanafunzi wengine waliomkejeli Kiambi.

Hadithi nyingine yenye inatoa onyo kwa watoto ni *Ndoto ya Mwanafunzi* na Manji (2013), Vijana wawili Juma na Hamisi waliojaribu kuwa mastowaways ili kuenda Bara Uropa waliambulia patupu baada ya kupatikana na kutiwa kifungoni kule Mauritius. Hili ni onyo kwa watoto wanaoweza kuwa na mafikira ya aina hii. Wanapata onyo kwamba, mosi, kule kujificha chomboni kuna madhara ya kiafya kutokana na kupumua gesi hatari zinazotoka kwa injini ya chombo hicho. Pili, ni hatia kujaribu kuabiri chombo bila idhini na kila mhalifu wa aina hiyo akipatikana, anapata adhabu ya kufungwa jela kama Juma na Hamisi. Kupitia kisa hicho cha watoto stowaways, mtoto msomaji atajiambaa na uhalifu wa aina hiyo ili asije akajitia matatani.

**Fasihi Andishi ya Watoto Hushauri**

Hivi karibuni Nchini Kenya na kwingineko Barani Afrika, pamekuwa na ripoti za kuatua moyo kuhusu kujitoa uhai kwa watoto na pia ujauzito kwa watoto wadogo walio katika shule za msingi na za upili (Musembi, 2022). Usawiri wa changamoto hizi unaonyesha uozo uliokithiri katika jamii yetu inayobadilika. Changamoto zinazomkumba mtoto wa kisasa mara nyingi humpelekea mtoto kukata tamaa. Ukataji tamaa huwapelekea baadhi ya watoto kujitia kitanzi, kutoroka nyumbani au kukumbwa na ugonjwa wa kiakili maarufu kama *depression.* Haya ni masuala nyeti ambayo hayapaswi kunyamaziwa. Miongoni mwa njia ambazo zinaweza kuchochea

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924

zinduko kwa watoto kuhusiana na changamoto zinazowakumba ni kupitia usomaji wa fasihi andishi yao inayoangazia changamoto hizi na namna ya kukabiliana nazo. Baadhi ya vitabu vya fasihi ya watoto humulika changamoto ambazo humkumba mtoto katika jamii ili ziweze kurekebishwa na wanaohusika. Kupitia fasihi, jamii humulikwa katika nyanja mbalimbali hususan nyanja ya kijamii, kisiasa, kidini kiuchumi na hata kitamaduni. Umuhimu wa makala hii ni kubainisha kuwa, kupitia fasihi andishi ya watoto, msomaji mtoto anaweza kufafanukiwa na hali halisi ya maisha yake na wakati huo huo kupata suluhu ya kutatua matatizo yanayomkumba na ya jamii yake. Vitabu vingi vya fasihi ya watoto ya Kiswahili hushauri mtoto kuhusiana na matatizo yanayomkumba maishani. Ushauri huu humpelekea mtoto kuelewa mazingira yake ya nyumbani na ya jamii pana anamoishi. Aidha, vinamsaidia mtoto kupata suluhu la baadhi ya changamoto anazokumbana nazo akiendelea kukua.

Kitabu cha watoto *Alitoroka Kwao* (2001) cha A. Mdari kilinuiwa kushauri mtoto hasa wa kike kuhusiana na tabia hasi ambazo anazibwia kutoka kwa marafiki wapotovu. Katika kitabu hiki, mhusika mkuu Eva ni msichana wa miaka kumi na mitatu. Kutokana na malezi mabaya ya babake wa kambo, anaamua kutoroka nyumbani kwenda jijini Nairobi. Kule jijini anakumbana na hatari nyingi kwa sababu hamjua jamaa yeyote katika jiji hilo. Anapata kazi ya uyaya kutangamana na marafiki wasichana ambao pia ni mayaya. Hatimaye wanampotosha licha ya kwamba mwajiri wake Bi. Mdamu alikuwa akimuonya kujiepusha na marafiki hao waovu. Anatoroka kwa mwajiri wake na kutafuta kazi kwenye baa na vilabu vya kuuzia pombe. Ankutana na Joni ambaye wanaanza kuishi pamoja kama mke na mume lakini baada ya miezi michache wanafarakana. Baadaye Eva anapashwa habari kuwa Joni ni mtu hatari na ana virusi vya Ukimwi na kwamba kafiwa na wake zake watatu kwa sababu ya maradhi hayo. Baadaye anamalizia kufanya kazi katika makao ya watoto mayatima baada ya kubainika kuwa hata yeye kaambukizwa virusi vya ugonjwa huo.

Kupitia usomaji wa kitabu hiki, mtoto anapata ushauri wa mambo matatu. Mosi, kutoroka nyumbani na kuelekea jijini ambapo hana jamaa na marafiki wanaompenda wa kuishi nao hakufai. Ni hatari. Ushauri anaopata ni kwamba, afadhari kuishi na jamaa na kusoma ili baadaye akienda jijini, anaweza kujikimu yeye mwenyewe kupitia kazi anayopata baada ya kusoma. Pili, kuna marafiki ambao hawafai. Wanapotosha mtoto na anaweza kujipata katika hali mbaya kama ya Eva ya kuambukizwa ugonjwa usio na tiba kama Ukimwi. Mtoto msomaji anashauriwa kujiambaa na marafiki kama hao. Tatu, mtoto wa kike anashauriwa kujiambaa na baadhi ya kazi kama uuzaji pombe katika vilabu. Kazi hii ni hatari kwamni kupitia kwayo, anaweza kupatana na wanaume hatari kama Joni na kuhatarisha maisha yake. Nnne, mtoto msomaji anapata ushauri kwamba, ni vizuri kusikiliza ushauri wa wakubwa wake. Eva alikuwa ameonywa na Sista Agatha na pia na mwajiri wake wa kwanza Bi. Mdamu. Kutokana na mapuuza yake, anaambulia matatizo chungu nzima kule jijini. Ushauri huu kupitia usomaji wa kitabu hiki una nguvu za kukongomelea katika akili ya mtoto msomaji hadi utu uzima wake.

Kitabu cha *Tumaini* pia kinatoa ushauri kwa watoto hasa wasichana kuhusiana na ukeketaji, ndoa za mapema na kukosa elimu. Mwandishi Momanyi anafanya hivyo kupitia mhusika mkuu Tumaini. Tumaini alifanya uamuzi wa maana alipotorokea kisu cha ngariba na kuamua kwenda kuishi na mamake mdogo ambaye ni mwanaharakati wa kutetea watoto wa kike. Tumaini alitaka kusoma. Hakutaka kukeketwa na kuachishwa masomo katika umri wake mdogo huo. Dada zake Mashaka na Rehema walioamua kukeketwa waliozwa wakiwa wadogo na wakaishia kupatwa na matatizo mengi sana ya uzazi na katika ndoa zao. Wamekosa pia matumaini ya maisha mazuri kwa sababu hawana kisomo kama Tumaini. Ushauri anaotoa Mwandishi kwa mtoto msomaji hasa msichana ni kwamba, elimu ni nzuri. Hubadilisha maisha ya mwanamke. Pili, mila na tamaduni zilizopitwa na wakati mathalan ukeketaji na ndoa za mapema ni potovu. Hazifai katika ulimwengu wa sasa.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924

Zinapaswa kupigwa kwa vyovyote vile. Mwandishi anamtumia Bi. Halima mamake mdogo wa Tumaini kutomelea ushauri kwamba, ni heri kutorokea kwa watu au mashirika mbalimbali katika jamii ambayo husaidia watoto wanaolazimishwa kukeketwa na kuozwa mapema. Lau Mashaka na Rehema wangefuata nyayo za Tumaini, maisha yao hayangekuwa ya kusikitisha na ya majuto kama yalivyo. Masaibu ya Mashaka na Rehema yanaweza kuzua ukata tamaa kwao. Kwa kusoma kitabu cha *Tumaini*, mtoto msomaji wa kike anapata ushauri mwafaka sana ambao labda hangeupata mahari pengine popote pale.

Riwaya ya watoto *Siku ya Wajinga* (2005) cha Momanyi vilevile ni mfano mzuri wa vitabu vya fasihi ya watoto ya Kiswahili ambavyo vinatoa ushauri kwa watoto. Kitabu hiki kinammulika muhusika mtoto kwa jina Zito ambaye ni mtundu na mwenye mizaha tele. Ni mwanafunzi katika shule ya msingi ya Kambini. Zito hana bidi masomoni. Ni mvivu pia na mienendo yake inamtia matatani kila mara na kusababisha aadhibiwe na wazazi wake na walimu mara kwa mara. Zito ana falsafa kwamba 'werevu ukikushinda jaribu ujinga'. Katika kutetea falsafa yake hii, Zito anafanya juhudi kuwashawishi wanafunzi wenzake kuamini kwamba, mtu mwerevu daima humtumikia mtu mjinga. Kutokana na utundu wake, anaishia kupata majeraha mabaya ambayo yalimpelekea kulazwa hospitalini. Aidha, utundu wake unampelekea kutimuliwa shuleni na hatimaye kujipata katika shule maalum ya kurekebisha tabia za watoto watundu. Tunaambiwa baada ya miaka miwili akiwa katika shule hii, Zito anagundua kwamba falsafa yake ya kuukumbatia ujinga haiwezi kumsaidia. Anarekebisha tabia na aliporudi katika shule yake ya zamani ya Kambini anaiaga falsafa yake na kuibuka na nyingine kwamba 'Ukitaka cah Mvunguni, sharti uiname'. Lakini wenzake tayari walikuwa wamekwisha kupiga hatua masomoni na kujiunga na shule za upili. Kitabu hiki kinatoa ushauri kwa mtoto msomaji kwamba, utundu haufai. Una madhara si haba. Huumiza. Zito licha ya kuumia na kujipata katika shule ya waarifu pia alichelewa kusoma. Wenzake wakaendelea na masomo yao vizuri hadi shule ya upili yeye akiwa bado shule ya msingi. Huu ni ushauri mwafaka ambao unampelekea mtoto kujiambaa na utundu maishani hata akiwa mtu mzima.

**Fasihi Andishi ya Watoto Hubadilisha Mielekeo Hasi ya Watoto**

Chochote mtoto husoma, hukongomelea katika akili yake hadi utu uzima wake. Mtoto anaposoma kitabu cha hadith ya *Safari ya Sungura*, cha Omusikoyo (2021), anaelimishwa kuhusiana na matatizo yanayotokana na tabia ya uvivu na utundu. Katika hadithi hii, Sungura ambaye ni muhusika mkuu anatoroka kwao ili aepuke kufanya kazi za nyumbani. Kulingana na Sungura, alihitaji kuishi mahali ambapo atakaa tu bila kufanya kazi yoyote. Alitaka kuishi mahali ambapo anakula na kucheza tu na wenzake. Alipotoroka kwao na kuenda kwa akina Kobe, Nyani na Fisi, aliambulia kukosa chakula na kukosa nguvu za mwili. Ilibidi arudishwe kwao alipounguzwa vizuri na wawazi wake na kula shibe yake kama ilivyokuwa awali. Hadithi hii itambadilisha mtoto msomaji kutoka kwa mielekeo hasi hadi kwa mielekeo chanya iliyo na faida katika maisha yake.

## HITIMISHO

Makala hii iliazimia kuchunguza nafasi muhimu ya fasihi andishi ya watoto ya Kiswahili kama mkakati wa malezi katik dunia ya Kisasa. Lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza ni kwa kiwango gani na kwa namna gani waandishi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto inawasaidia watoto kupitia majukumu ya fasihi hiyo kwa mtoto msomaji. Makala hii imemulika dima ya fasihi andishi ya watoto katika kuwaelimisha, kuwatahadhalisha, kuwaonya na kuwapa ushauri wanapoendelea kukua. Aidha, kwa kusoma vitabu hivi, mtoto anapata kufahamu maadili ambayo jamii yake inatarajia awe nayo ili kujiepusha na tabia hasi ambazo hatima yake si nzuri. Fasihi ya watoto kupitia makala hii inaonyesha kutoa mchango mkubwa katika kukuza maarifa na ukweli katika maisha ya mtoto. Hii ni kutokana na sababu kwamba, fasihi ya watoto imekuwa nyenzo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1924

muhimu ya kuwasaidia watoto kuelewa mazingira yao na kuibua mwonoulimwengu wao katika dunia inayobadilika kila uchao. Hadithi wanazosoma huifadhiwa katika kumbukumbu zao maishani mwao. Hii ni kutokana na sababu kwamba, watoto hubwia wanachosoma kuwa kweli na huwa na taathira katika maisha yao ya baadaye. Makala hii inapendekeza kwamba waandishi wa fasihi ya watoto ya Kiswahili wajaribu kuandika kazi nyingi zinazo waadilisha watoto, kuwaonya, kuwashauri na kuwaelimisha namna ya kukabiliana na mazingira yao. Kwa kufanya hivyo, fasihi andishi ya watoto itakuwa katika mstari wa mbele katika kutoa mchango wake kwa malezi ya mtoto katika jamii ya sasa.

**MAREJELEO**


Hunt, P. (1991) Criticsm, Theory and Childrens's Literature. Oxford: Blackwell.

Manji, A. (2013) Ndoto ya Mwanafunzi: Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation.

Matundura, B. (2007). Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mbuthia, E. M (2018). The Role of Children's Literature in Fomulating their World View in *International Journal of Education and Research*. Vol 6. No. 2 Feb. 2018.

Mdari, A. (2001) *Alitoroka Kwao*. Nairobi: Focus Books.

Momanyi, C. (2006) *Tumaini*. Vide-Muwa: Nairobi

Momanyi, C. (2005) *Siku ya Wajinga*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Musembi, N. (2022). Ukataji Tamaa miongoni mwa Watoto katika jamii ya Kisasa. Tathmini kutoka Riwaya ya Kiswahili. Katika Jarida la CHAKAMA Juzuu 1 uk 141-147.

Musembi, N. N. (2018). "Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii Inayobadilika Karne ya 21". Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la Kimataifa la Chaukidu, SUZA.

Musembi, N.N (2009). *Nipe Sababu*. Nairobi: Oxford University Press.

Musembi, N.N. (2019). Dhiki Yangu. Naorobi. East African Educational Publishers.

Mwanzi, H. (2006) "Children's Literature: The Concept of Socializing the Young" In the Nairobi Journal of Literature No 4. pp 49.

Ndungo, C. (1985) "Matumizi ya Tamathali za Usemi katila Lugha ya Kisasa". Katika Njogu, K. na wengineo (Wah.). *Fasihi simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications.

Ngugi, P.M. (2003). *Usicheze na Moto*. Nairobi: Oxford University Press.

Ngugi, P.M. Nabea, W. (2011). Children's Literature in Kiswahili: A Stylistic Approach katika *East African Literature: Essays on Written and Oral traditions*, Logos Verlag Berlin. Kur. 223-244.

Omolo, O. (1971) *Uhalifu Haufai*: Longhorn Publishers Ltd.

Omusikoyo, T. (2021). Safari ya Sungura: Nairobi: Story Moja Publishers.

Ngugi, P.M (2016). Usawiri wa Masuala Ibuka katika Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Kenya katika: *Mulika*, No 35. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 76-86.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.


 | This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.